HOSTEL NA USAFIRI

Wanafunzi wetu huishi katika hosteli nzuri zinazosimamiwa na Mapadri na watawa. Shule ina usafiri kwa ajili ya wanafunzi katika safari zote za ndani na hata nje ya shule.

USAJILI WA WANAFUNZI

Shule imesajiliwa mnamo mwaka 2017 kwa namba ya usajili S5616. Shule inapokea wanafunzi wa kike na wa kiume wanahitaji kujiunga na kidato cha kwanza. Ili kujiunga mwanafunzi atatakiwa kufanya mtihani wa usahili (interview).

NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Shule ya Sekondary ya Seminari Fransalian Hekima ipo Maji ya Chai—Arusha, barabara ya kuelekea Kitefu.



Knowledge & Wisdom

MAWASILIANO

Fransalian Hekima Seminary Secondary School

P. O. Box 126, Usa River-Arusha.

Simu: +255 621489222, +255 759895862

Barua Pepe:fransalianhekimaschool@gmail.com

FRANSALIAN HEKIMA SEMINARY SECONDARY SCHOOL

P. O. Box 126, Usa River
Arusha – Tanzania

OUR VISION:

Fransalian Hekima Seminary Secondary School is to strive for academic excellence for the integral growth of the young and to mould them into value based responsible citizens to build up a nation guided by Wisdom and Benovelence.

OUR MISSION:

Fransalian Hekima School commits itself to an overall development of personality of pupils by providing an ambience of intellectual pursuit and character formation through study and co-curricular activities.

FRANSALIAN HEKIMA ni Shule ya Bweni ya wavulana na wasichana iliyopo chini ya Wamisionari wa Shirika la St. Francis de Sales. Shule ilianzishwa mwaka 2018 katika jiji la Arusha. Shule inafundisha masomo ya Sayansi, biashara na sanaa.

KITAALUMA

Shule ina matokeo mazuri kwa mitihani ya ndani na ya nje. Kila mwanafunzi hupewa fursa ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kitaaluma na hivyo kumwezesha kufikia malengo yake.

WALIMU

Shule ina walimu wa kutosha wenye taaluma nzuri ya ufundishaji, wenye maadili mema na uzoefu wa kutosha.

UTAMADUNI

Shule hutoa fursa kwa wanafunzi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiutamaduni ikiweno maigizo, uimbaji, vichekesho, ngoma za asili, ngonjera na jaiving. Shule imeshiriki katika mashindano ya kiutamaduni na kujipatia tuzo kedekede.

MAADILI

Shule inaongozwa na Watawa wa Shirika la Missionaries of St. Francis de Sales na kusimamiwa na shirika la masista wa 'Congregation of the Mother of Carmel', hivyo huwalea watoto katika misingi ya maadili mema yenye kumfanya mwanafunzi afikie malengo yake.

KIROHO

Shule hutoa semina mbalimbali za kiroho zenye kumuwezesha mwanafunzi kukua kiroho na kumpenda Mungu. Vilevile shule hutoa huduma za ushauri wa kisaikolojia ili kumfanya mwanafunzi ajiamini katika kila somo na kila hatua anayopiga. Kila siku wanafunzi wote hushiriki Misa Takatifu na ibada mbalimbali.

MICHEZO

Shule ina viwanja vizuri vya michezo kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika Nyanja mbalimbali za kimichezo. Shule ina siku maalumu za michezo na mashindano.

MAKTABA

Shule ina maktaba nzuri yenye vitabu vya kutosha na usimamizi mzuri kumwezesha mwanafunzi kujiandaa vyema kitaaluma.

MAABARA

Shule ina maabara kubwa za kisasa kwa masomo ya sayansi (Physics, Chemistry, Biology) na Computer.

BENDI YA SHULE

Shule ina bendi nzuri yenye vifaa vya kisasa na usimamizi thabiti. Lengo ni kuburudisha, kuhamasisha, kukuza vipaji, kuwaimarisha vijana na kuwafanya wakakamavu.